BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 20 Mei, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

270. MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (Jimbo la Wete) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Jimbo la Wete ni kati ya majimbo yaliyobahatika kuwekwa taa za barabarani zisizopungua 170 ambazo zimetumia fedha nyingi za Serikali. Hata hivyo, ni takriban taa tisa hadi kumi na tatu zinazowaka kwa sasa na zilizobakia zimekuwa kama pambo la barabarani.

(a) Je, Serikali ina mpango gani utakaohakikisha taa hizo zinafanyiwa ukarabati na kuwaka.

(b) Je, Serikali imetumia kiasi gani cha fedha katika ujenzi wa taa za barabarani zilizowekwa katika jimbo la Wete.

361. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Sheria ya Tawala la Mikoa inawatambua Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwa ni Watumishi wa Umma, na Sheria ya Utumishi wa Umma Nambari 2 ya 2011 na Sheria Nambari 3 ya 2003, zote zimepiga marufuku kwa Mtumishi wa Umma kushiriki katika siasa na zimeweka utaratibu maalum wa namna ya mtumishi kushiriki katika siasa.

(a) Je, ni kwa nini Wakuu wa Mikoa na Wilaya wanajihusisha na siasa waziwazi.

(b) Je, ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa uvunjaji wa masharti ya sheria hizo.

## <u>Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora</u>:

85. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Katika kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar iliandaa Kongamano zuri sana la Kiimani kwa Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambalo lilizinduliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Miongoni mwa mada zilizowasilishwa ni Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji wa Viongozi kwa Umma.

(a) Je, kutokana na Kongamano hilo, ni lini Serikali itabadilisha na kuandika upya Sheria ya Viapo na Hati za Uteuzi nambari 1 ya mwaka 1996, ili kuwataka Viongozi kuapa Kiapo cha Uaminifu pamoja na Kiapo Mahususi cha Maadili na Uwajibikaji.

(b) Kwa kuwa Kongamano hilo lilileta matokeo mazuri ya kuwakumbusha viongozi wajibu wao, ni lini Serikali itaitisha tena makongamano kama hayo kila mara kupitia Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar.

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

138. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Je, Serikali imeweka mikakati gani ya kifedha inayohakikisha wananchi wa vijijini wanafaidika na ukuaji wa uchumi wa nchi.

169. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) umeendelea kuwekeza katika ujenzi wa miradi mbalimbali Unguja na Pemba, huku baadhi ya miradi hiyo ikishindwa kuleta tija iliyokusudiwa na kusababisha hasara kubwa kwa mfuko huo, hali inayotia wasiwasi kwa wanachama wake wanaowekeza pesa zao ili ziwafae baada ya kustaafu.

(a) Ni ipi sababu kuu iliyoufanya Mfuko huo kuamua kuingia katika sekta ya uwekezaji wa ujenzi wa miradi ya kibiashara.

(b) Je, ni kiasi gani cha uzalishaji wa faida kimepatikana katika baadhi ya miradi inayofanya kazi kwa sasa na faida hiyo inawanufaisha vipi wanachama wake.

(c) Je, Serikali ipo tayari kuleta marekebisho ya Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamiii Zanzibar ili kutoa fursa kwa mifuko mengine kuja kuingia katika soko la ushindani hapa Zanzibar.

**Wizara ya Kazi na Uwekezaji:**

96. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Pamoja na juhudi kubwa na nzuri za Serikali ya Awamu ya Nane ya kuvutia wawekezaji katika sekta mbalimbali, bado maeneo mengi yenye uwekezaji huo hasa vijijini, hali za wananchi wake ni duni, makaazi yao sio bora na baadhi ya huduma za jamii zipo kwa kiwango cha chini sana. Hali hii inamaanisha kuwa uwekezaji katika maeneo yao hauwanufaishi vya kutosha, hata ajira zinazotolewa katika maeneo hayo zinatolewa zaidi kwa wageni.

(a) Je, kuna mpango gani wa kubadilisha sera ya uwekezaji kwa kuwezesha eneo lenye uwekezaji mkubwa kupatiwa asilimia fulani ya mapato ya uwekezaji ili kuinua hali za maisha ya wananchi katika eneo husika.

(b) Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuelekeza nguvu zake

vijijini na kuhama mjini, kwa kujenga makaazi bora ya wananchi yanayolingana na mazingira yao hata kama sio ya ghorofa.

(c) Kwa nini Serikali haioni haja ya kupeleka uwekezaji katika maeneo kulingana na shughuli za kiuchumi za eneo husika, mfano maeneo yenye uvuvi wakaweka uwekezaji wa viwanda vya uvuvi na kilimo wakapeleka viwanda vya kusindika mazao.

<u>**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**</u>

29. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha miundombinu ya barabara katika maeneo tofauti ya nchi, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa kukuza uchumi na kurahisisha kupatikana huduma kwa wananchi. Hata hivyo, kutokana na ukuaji wa kasi wa Mji wa Chake Chake na ongezeko la ujenzi wa makaazi mapya katika maeneo ambayo awali hayakuwa na miundombinu ya barabara za kudumu, kumejitokeza changamoto ya kukosekana kwa miundombinu hiyo muhimu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara mpya katika maeneo mapya ya makaazi ya Mji wa Chake Chake, hususani maeneo ambayo hayakuwa na miundombinu ya kihistoria ya barabara, ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za usafiri na kuchochea maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

71. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Serikali ya Awamu ya Nane imefanya juhudi kubwa za kujenga miundombinu ya barabara na kwa kufanya hivyo baadhi ya nyumba na maeneo ya biashara ya wananchi yamelazimika kuvunjwa ili kupisha utanuzi wa barabara. Hata hivyo, yapo baadhi ya maeneo ambayo wananchi wamevunjiwa yakiwa nje ya kipimo cha mita 15 cha barabara. Maana yake wapo nje ya hifadhi ya barabara kwa mujibu wa sheria na fidia waliyostahiki kulipwa, inadaiwa kuwa ndogo.

(a) Je, ni vigezo gani vinatumika kuwalipa fidia wananchi wanaovunjiwa hasa wale ambao barabara imewafuata baada ya utanuzi.

(b) Kwa kuwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Barabara ya mwaka 2014 imeongeza mita 15 na zipo barabara

zimetanuliwa kufika maeneo ya watu, kwa nini Serikali isije na mpango wa kuwapatia wananchi hao makaazi mbadala, badala ya kuwalipa fedha kidogo ambazo hazitoshi kutafuta kiwanja na kujenga makaazi mengine.

**<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>**

175. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Miji yote iliyoendelea ulimwenguni ni zao la sera ya kusimamia vizuri mipango madhubuti ya utumiaji wa ardhi zao pamoja na kuwa na mipango bora ya kuitumia Miji vizuri (*Site Planning*), ingawa kwetu sisi Zanzibar hali ipo tofauti. Serikali haijafanikiwa vya kutosha kupima na kutoa *site plan* kwa mji wote wa Zanzibar, hali inayopelekea kuongezeka kwa migogoro mingi ya ardhi hapa nchini kutokana na ujenzi holela wa wananchi wetu.

(a) Kwa nini Serikali haijafanikiwa vya kutosha kuweka mkakati maalumu juu ya maendeleo ya maakazi katika miji yetu ya Zanzibar.

(b) Ni ipi ahadi ya Serikali kwa wazanzibari juu ya kuanzisha mchakato wa upimaji wa ardhi kwa maeneo yote ya Zanzibar.

(c) Kwa kuwa Serikali haijafanikiwa vya kutosha katika wajibu wake huu, je ipo tayari kuziruhusu kampuni binafsi kufanya kazi hiyo ya kupima ardhi na kutoa *site plan*.

**<u>Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:</u>**

92. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Baada ya kazi nzuri ya ujenzi wa viwanja vya michezo katika kila Wilaya ikiwemo katika jimbo la Paje, ambapo wananchi walitoa eneo lao ili kujengwa uwanja wa michezo ambao walikuwa wakiutumia bure wakati wote, hivi sasa, viwanja hivyo wamepewa wawekezaji ili kuviendesha, huku bila ya shaka kukitarajiwa kuwepo kwa gharama za watumiaji ili kuleta tija ya uwekezaji huo.

(a) Je, madhumuni ya ujenzi wa viwanja hivyo ni kwa ajili ya biashara (uwekezaji) au kukuza michezo na kuimarisha afya za wananchi wetu.

(b) Kwa wananchi waliotoa maeneo yao kujengwa viwanja hivyo,

huku wao walikuwa wanavitumia bure kama ilivyokuwa kwa jimbo la Paje, je, watawekewa utaratibu upi wa kuvitumia viwanja hivyo.

(c) Je, Wizara imefanya utafiti wowote na kujua uwezo wa vilabu na jamii zetu kumudu gharama za kukodi viwanja hivyo.

## Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

122. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa hivi karibuni Serikali imechukua hatua ya kuviondoa vyuo vinavyotoa fani za kitaalamu kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na kwa kuwa vyuo hivyo ni Chuo cha Uwalimu Nkrumah, Chuo cha Utalii Maruhubi na vyenginevyo. Na kwa kuwa vyuo hivyo viliunganishwa na SUZA kwa utaratibu wa kisheria kupitia Sheria namba 7 ya mwaka 2016 (Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar).

(a) Kwa nini utaratibu wa kuviondoa vyuo hivyo kutoka SUZA haukutumia sheria kama ilivyotumika wakati wa kuviunganisha.

(b) Kwa kuwa vyuo hivyo vimeshaanza kufanya shughuli zake nje ya SUZA, wakati Sheria namba 7 ya mwaka 2016 bado inavitambua vipo SUZA, kwa nini Wizara haioni kuwa inavunja sheria halali iliyotungwa na Baraza hili.

(c) Kama uamuzi wa kuviondoa SUZA umeshafanyika, kwa nini Sheria namba 7 ya mwaka 2016 isiletwe Barazani kufanyiwa marekebisho au kufutwa ili kuviondoa vyuo hivyo kisheria.

## Wizara ya Afya:

433. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Hivi sasa kumeanzishwa utaratibu wa utumiaji wa tokeni namba kwa wagonjwa wanaofika kupata huduma za afya katika hospitali zetu.

Je, kuna mkakati gani wa kuwasaidia wagonjwa wa dharura na wale wanaokwenda kliniki kupata huduma za afya.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

38. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kuna eneo karibu na Amana Benki katika Mji Mkongwe ambalo linamilikiwa na mtu binafsi na ambalo limekodishwa kwa kampuni moja kufanya biashara ya maegesho kinyume na sheria.

(a) Sheria gani imetumika kuchukua eneo la mtu binafsi na kulikodisha kwa kampuni binafsi kufanya biashara ya maegesho bila ya ridhaa ya mmiliki wake.

(b) Je, kuna fidia yoyote mtu huyo anaweza kulipwa kwa kuchukuliwa eneo lake na kupewa mtu binafsi kufanya biashara ya maegesho.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

499. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Mfumko wa bei unaweza kuchochewa sio tu na sababu za ndani, bali pia na misukosuko ya kiuchumi ya kimataifa hali inayoweza kuathiri moja kwa moja uchumi wa Zanzibar na maisha ya wananchi.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na athari za misukosuko ya uchumi wa dunia inayochangia kuongezeka kwa mfumko wa bei nchini.

(b) Je, Serikali imeweka hatua gani za kuimarisha uthabiti wa soko la ndani.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

313. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Kumekuwepo na ongezeko la changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana, hususan wahitimu wa vyuo vikuu na vyuo vya kati, hali inayosababisha ongezeko la utegemezi katika jamii.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani mahsusi wa kuzalisha ajira endelevu kwa vijana, hususan wahitimu wa vyuo vikuu na vyuo

vya kati.

(b) Ni hatua zipi ambazo Serikali imechukuwa kuzalisha ajira za staha na zenye tija kwa vijana wa Zanzibar.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

215. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe):
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Katika hali tuliyoizoea, inapotokezea kesi ya ubakaji baina ya mwanamme mwenye miaka 20 amemuingilia kwa makubaliano na mwanamke wa miaka 20, mwanamme huyo peke yake hufunguliwa mashtaka, hutiwa hatiani na kutumikia kifungo inapotokezea mwanamke huyo kudai kubakwa.

Kwa nini sheria zilizopo hazifanyiwi marekebisho ili mwanamke aliyeshiriki katika tendo akashtakiwa kama mwanamme.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Afya:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**20 Mei, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**